**Maswali ya mara kwa mara: Ni sera zipi 4 za USCIS zilizoghairiwa na Mahakama?**

***Habari hii ni ya ufanisi kutokea 06/11/2026 na inauwezekano wa kubadilika-hakiki tena sasisho!***

***Hii ni kwa kukufahamisha tu na isichukuliwe kama ushauri wa kisheria***

## Sasisho muhimu: Uamuzi wa mahakama kuhusu sera za USCIS.

Mnamo Juni 5, 2026, Hakimu wa serikali kuu alitoa uamauzi kuhusu sera za USCIS ambazo zimeweza kupunguza,kusimamisha au kuzuia kesi za uhamiaji kwa waomba hifadhi na watu kutoka mataifa 39 ambao Marekani imewaita "wenye hatari kubwa"(rejelea *Dorcas International Institute of RI v. USCIS*). Haya ndiyo unayotakiwa kujua

## Hakimu aliamua vipi?

Hakimu alsema kuwa USCIS **ilitenda kinyume** kwa kuweka sera nne zilzosimamisha au kupunguza usindikaji wa uhamiaji kwa misingi ya uraia hasa kwa watu wanaotoka mataifa 39, na alaimua USCIS **kukoma** kutumia sera hizi nne. Mataifa 39 ni: Afghanistan, Angola, Antigua and Barbuda, Benin, Burkina Faso, Burma, Burundi, Chad, Cote d'Ivoire, Cuba, Dominica, Equatorial Guinea, Eritrea, Gabon, Haiti, Iran, Laos, Libya, Malawi, Mali, Mauritania, Niger, Nigeria, Republic of Congo (Brazzaville), Senegal, Sierra Leone, Somalia, South Sudan, Sudan, Syria, Tanzania, The Gambia, Togo, Tonga, Turkmenistan, Venezuela, Yemen, Zambia, Zimbabwe na watu wanaotumia hati za mamlaka ya Palestina

## USCIS iliamuliwa kufanya nini kuhusu sera zilizoghairiwa?

USCIS iliamuriwa:

- **kuanza zindikizo za maombi ya hifadhi** na kusimamsha kuondolewa kwa raia wa mataifa yote.
- **Kuondoa kusimamishwa** kwa maombi ya uhamiaji kutoka watu wa kutoka mataifa 39. USCIS lazima ianzishe mchakato wa usindikaji wa maombi na kutoa ruzuku za uhamiaji, ikwemo green cards, vibali vya kazi,hati za usafiri na uraia kwa watu kutoka mataifa lengwa 39.
- **Kukomesha kufungua tena na kukagua upya** kesi zilizokuwa tiyari zimeamuliwa na kupitishwa kwa watu kutoka mataifa 39 walioingia Marekani baada ya Januari 20, 2021, kwa misingi tu ya uraia.
- **Kutotumia uraia wa nchi iliyoteliwa kama sababu hasi** wanapoamua maombi fulani.

## NI nini HAKIBADILIKI?

Uamuzi wa mahakama **HII HAU**:

- Kukomesha **makataa ya usafiri** yaliyopo ,kunyima **visa** za usafiri kwa raia wa mataifa 39"wenye hatari kubwa na raia wa mataifa 75"zindizo la umma" kusafiri Marekani.
- Kuanzisha usindikaji wa **maombi ya kubadilisha hadhi ya ukimbizi(green card)**.
- Kuanzisha **mpango wa hifadhi za ukimbizi** ambayo kwa sasa inahudumia tu raia weupe kutoka Afrika ya Kusini.
- Kubadilisha **sera zingine zozote za USCIS au sera za Idara ya Serikali**.

## Ni nini kitatokea baadaye?

USCIS imekata rufaa, lakini ilisema itafuata maagizo pale inaposubiria rufaa. Hii inamaanisha kuwa, kwa sasa, USCIS ita:

- toa uamuzi kuhusu green cards, vibali vya kazi, hati za usafiri.uraia ,na maombi mengine yaliyokuwa yamasimamashwa
- Panga upya tarehe ya sherehe za kiapo cha uraia ambazo zilighairiwa
- Thibitisha upya michakato iliyofunguliwa upya kwa sababu tu za uraia wa mhusika.
- Kukomesha kutumia misingi ya uraia kama sababu za kunyima ruzuku, kama vile kibali cha kazi

## Ni nini pia chaweza kutokea?

USCIS inaweza kuomba mahakama ya rufaa kusimamisha agizo la mahakama ya chini Mahakama ya rufaa inaweza:

- Inaweza kuweka agizo lile lile la mahakama ya chini, **au**
- Kusimamisha agizo, inayoipa USCIS nafasi **kuendeleza sera nne zenye changamoto** hadi rufaa imekamilika

**Nina maswali bado kuhusu mchakato wangu. Ni nina ninaweza kuuliza ?**

Kama unaamini mabadiliko haya yanakulenga au una maswali kuhusu chaguzi zako,unapaswa kuwasiliana na mtoa huduma za uhamiaji aliyeidhinishwa. Rejelea hapa chini kupata huduma za kisheria na ushauri.

| | | |
|---|---|---|
| Mtandao wa watetezi wa uhamiaji “**Immigration Advocates Network**” | Chama cha wanasheria wa uhamiaji wa Marekani ”**American Immigration Lawyers Association**” | Orodha ya ASAP ya wanasheria binafsi “**ASAP list of private attorneys**” |